# CHUO KIKUU MAARUFU DUNIANI

Ninafahamu wewe unajua vyuo vikuu vingi vilivyopo hapa nchini na nje ya nchi pia. Katika maisha yangu sitasahau maisha ya chuo kikuu kimoja kinachoitwa chuo cha GONGA KWA NGUVU. Je uliwahi kulisikia jina hili mahali popote?

Basi wewe endelea kusoma tu halafu utakifahamu vizuri chuo kikuu hiki.Kwa zaidi ya miaka kumi nilikuwa nikisoma katika chuo kikuu hiki.

Hiki ni chuo cha maisha magumu na taabu sana.Nilikuwa ninafanyakazi katika kiwanda kimoja hapa nchini. Nilikuwa ninafanya kazi kutoka saa kumi na mbili jioni hadi saa mbili asubuhi yake. Yaani usiku kucha aisee! we acha,we acha tu! Zaidi ya masaa kumi na nne

Ni afadhali ufanye kazi mchana lakini usiku hata muda wa kupumnzika hakuna. Utaniuliza kwani mchana watu hupumzika?

Nitakujibu ndiyo, “si ule muda kidogo wa kwenda kula”.

Mwenye kiwanda ameweka lengo ambalo lazima mlifikie endapo mambo yanakwenda bila shida yoyote. Yaani kama umeme haukukatika, au kama mitambo haikuharibika.

Mimi kuna kitu kilinikwamisha sana, kile kinachoitwa cheo. Kama ilivyo kawaida watu wengi wanapenda vyeo sana. Duuhh! mimi jamaa waliniweka kuwa msimamizi wa watu karibu arobaini hivi.

Mwanzoni nilikuwa ninasimamia watu zaidi ya hamsini. Maana yake kila ukipita kona hii unaitwa bosi. Kwa maana nyingine hewa yote imejaa jina bosi Sikayinda.Na zawadi kubwa ni shikamoo bosi nyingiii yaani dunia ni hadaa sana.Na hasa kama huna macho ya akili ya kukufanya ugundue ukweli wa maisha.Na hasa kama huna ujasiri wa kujigundua wewe mwenyewe.

Ingawa wafanyakazi walikuwa wanafanya kazi kubwa na ngumu na chini ya usimamizi.

Njoo sasa kwenye mshahara. Mshahara wa msingi ulikuwa ni shilingi za Kitanzania elfu nne na mia tano. Siyo kwamba ninazua au ninaamua kusema tu. Huo ndio ukweli wenyewe,huo ndio mshahara wa msingi halafu unaongezewa na wenzetu wanasema "OT" au kwa kirefu overtime. Yaani masaa ya ziada. Halafu eti na kahela kiasi cha shilingi mia mbili na hamsini eti usumbufu wa kufanya kazi usiku.Sijui kama umeelewa, eti kwa vile ulikuwa ulale na familia, lakini kwa vile wamekusumbua kuja kufanya kazi usiku basi wana kupa kiasi hicho.Hiyo ina kufanya wewe utoke na jumla ya shilingi za Kitanzania elfu saba na mia mbili. Kama kiwango cha chini kabisa. Huo si utani tu.

Hapo nimesahau kuna visenti eti vinaitwa maziwa. Kulikuwa shs, 400, 650, 750, 1000, 1200, 1950, 2100 na 2600 eti kutegemea na umuhimu wa mtu. Lakini mimi ninaona ni kutokana na maamuzi ya aliyepanga viwango hivyo.Hivyo ndivyo vinavyofanya upate jumla hiyo hapo juu ambayo ilitofautiana kadri ya kiasi cha maziwa.Mimi pamoja na wachache tulikuwa tunapata zaidi kidogo kwa sababu ya visenti hivyo vya maziwa ambavyo vilikuwa zaidi ya elfu moja na mia tano.

Sasa hapo ni usiku, lakini mkiingia mchana saa mbili asubuhi na kutoka saa kumi kamili jioni. Basi unapata elfu nne na mia tatu vile.Halafu unapata na maziwa, yaani vipesa fulani vile. Kadri ya vimaziwa nilivyoorodhesha hapo juu kiwango cha mwanzo ni elfu nne na mia saba. Kumbuka kuna matumizi ya nauli , chakula cha mchana. Wakati mwingine hata kupiga hesabu zenyewe ninaona uvivu. Lakini hayo ndiyo yaliyokuwa ni maisha ya chuoni, chuo changu kikuu cha **gonga kwa nguvu.** Inawezekana watanzania wengi wanasoma katika chuo hiki.